IDARA YA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI YA MISSOURI
KITENGO CHA HUDUMA ZA MASOMO – OFISI YA ELIMU MAALUM

# UTAFITI WA ELIMU MAALUM

## MAAGIZO

Mzazi Mpendwa,

Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari ya Missouri inathamini maoni ya wazazi wote katika shule za Missouri. Tutashukuru iwapo utatenga muda wa kujibu utafiti huu mfupi kuhusu huduma za elimu maalum ambazo mtoto wako hupokea. Utafiti huu ni wa siri; majibu yako hayashirikiwi na wilaya ya shule au mtu mwingine yeyote. Ni muhtasari wa majibu yote tu ndio hutolewa kwa wilaya za shule ili kusaidia shule zote kuboresha elimu ya watoto wetu. Unaweza kujaza utafiti huu kwa njia mbili; **(1)** mtandaoni, au **(2)** kwa kujibu maswali yaliyo hapo chini na kutuma utafiti kwa njia ya barua kwenye anwani iliyotolewa. **Tafadhali jaza utafiti huu kabla ya tarehe 31 Machi.** Asante sana kwa kutoa maoni yako.

**Kutuma kwa njia ya barua:** Unaweza kujibu maswali yafuatayo na kutuma hati hii kwa njia ya barua kwenye anwani ifuatayo:

Special Education Survey
University of Missouri – Institute of Public Policy
137 Middlebush Hall
Columbia, MO 65211

## MASWALI YA UTAFITI

**Wilaya:** **Msimbo wa Wilaya:**

| Tafadhali tia alama kwenye duara <u>moja</u> iliyo upande wa kulia wa kila swali. | Asili ya Kihispania/ Kilatino bila kujali mbari | Mwasia | Mwenyeji wa Hawaii au Mwenyeji Mwingine wa Kisiwa cha | Mwafrika au Mwamerika Mwafrika | Mwamerika Mhindi | Mzungu | Mbari Mbili au Zaidi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1) Onyesha aina **moja** ambayo inaeleza vizuri mbari au kabila la mtoto wako. | O | O | O | O | O | O | O |

| | Shule ya chekechea | Shule ya msingi (Madarasa Darasa la chekechea hadi darasa la 6) | Shule ya sekondari (Madarasa Darasa la 7 hadi 12) |
|---|---|---|---|
| 2) Mtoto wako yuko katika darasa la ngapi? | O | O | O |

| | Chini ya Mwaka 1 | Mwaka 1 hadi 2 | Miaka 3 hadi 5 | Miaka 5 au zaidi |
|---|---|---|---|---|
| 3) Mtoto wako amepokea huduma za elimu maalum kwa muda gani katika wilaya hii ya shule? | O | O | O | O |

| | Sikubali Kabisa | Sikubali | Sikubali wala Sikatai | Ninakubali | Ninakubali Kabisa |
|---|---|---|---|---|---|
| 4) Shule ya mtoto wangu huwapa wazazi mafunzo kuhusu masuala ya elimu maalum. | O | O | O | O | O |
| 5) Walimu na wataalamu wengine katika shule ya mtoto wangu wamenipa maelezo kuhusu mashirika ambayo huwasaidia wazazi wa wanafunzi wenye ulemavu. | O | O | O | O | O |
| 6) Shule ya mtoto wangu hueleza hatua ambazo wazazi wanaweza kuchukua iwapo hawakubaliani na uamuzi wa shule. | O | O | O | O | O |
| 7) Walimu na wataalamu wengine katika shule ya mtoto wangu wameomba maoni yangu kuhusu jinsi huduma za elimu maalum zinavyotimiza mahitaji ya mtoto wangu. | O | O | O | O | O |
| 8) Walimu na wasimamizi katika shule ya mtoto wangu hunihimiza nishiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi. | O | O | O | O | O |
| 9) Walimu na wataalamu wengine katika shule ya mtoto wangu huwasiliana nami kuhusu hatua ambazo mtoto wangu anapiga katika kutimiza malengo ya Mpango wa Elimu ya Binafsi (Individualized Education Program (IEP). | O | O | O | O | O |
| 10) Ninachukuliwa kama mshirika sawa na walimu na wataalamu wengine katika kupanga mpango wa mtoto wangu. | O | O | O | O | O |
| 11) Kuhusika kwangu katika elimu ya mtoto wangu kumeboresha mafanikio yake. | O | O | O | O | O |
| 12) Shule ya mtoto wangu huhimiza wazazi kuhusika. | O | O | O | O | O |
| ***Jibu swali lifuatalo iwapo mtoto wako ana umri wa miaka 16 au zaidi.*** | O | O | O | O | O |
| 13) Shule ya mtoto wangu hutoa maelezo kuhusu mashirika ambayo yanaweza kumsaidia mtoto wangu kujiunga na taaluma, mafunzo ya kiufundi au elimu ya juu baada ya kumaliza shule. | O | O | O | O | O |

Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, dini, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, utaifa, umri, hali ya mwanajeshi aliyestaafu, ulemavu wa kimwili au kiakili au kwa msingi mwingine wowote kulingana na sheria zilizo kwenye mipango na shughuli zake. Maswali yanayohusiana na mipango ya idara na eneo ambapo huduma, shughuli na vituo ambavyo vinaweza kufikiwa na watu wenye ulemavu vinapatikana, yanaweza kuelekezwa kwa Jefferson State Office Building, Director of Civil Rights Compliance and MOA Coordinator (Title VI/Title IX/504/ADA/ADAAA/Age Act/GINA/USDA Title VI), 5th Floor, 205 Jefferson Street, Sanduku la Posta 480, Jefferson City, MO 65102-0480; nambari ya simu 573-526-4757 au TTY 800-735-2966; barua pepe**civilrights@dese.mo.gov**.

MO 500-2986 (12-20) Swahili